# *Mara Moja Tu Zaidi, Bwana*

Hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa. Huku vichwa vyetu vimeinamishwa na mioyo yetu imeinamishwa mbele za Mungu, kufungwa kwa mkutano huu mkuu, yubile ambayo tumekuwa nayo hapa, na kwenye Neno la Bwana, sijui, usiku wa leo, ikiwa mioyo yetu haipasuki tu kwa ajili ya kitu kutoka kwa Mungu. Kama ndivyo, hebu tumwinulie tu Yeye mikono yetu, na kusema, tuseme tu, "Hii ndiyo haja yangu, Bwana. Unajua."

2 Baba yetu wa Mbinguni, angalia chini sasa juu ya mikono yetu. Mikono hiyo ikiwa imeinuliwa, inamaanisha kwamba tunasalimisha yote tuliyo nayo Kwako. Wewe unajua tunayohitaji, Baba, nasi tunaomba ya kwamba Wewe utakimu mahitaji yetu. Wakati mwingine matakwa yetu ni mengi kuliko mahitaji yetu. Lakini, Baba, Wewe hukimu mahitaji yetu, kwa sababu tunaweza kuomba hayo kwa imani. Uliahidi utafanya hivyo. Katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba hayo. Amina.

Sasa ketini.

3 Kwa Ndugu Moore, na Dada Moore, Ndugu Brown na nanii wake, Ndugu Lyle, Ndugu Boutliere, na watu hawa wote wazuri hapa wa kanisani, wadhamini, mashemasi, chochote kile walicho, kwa hakika nina shukrani kwa ajili ya fursa hii na wakati mwema ambao nimekuwa nao nikiwa hapa. Hawa waanzilishi mashuhuri waliokuja humu miaka iliyopita, wakiwa na vipande vya karatasi chini ya kiatu chao, na wametoa juhudi za kujitolea bila ubinafsi ili kuleta mahali hapa pa kuabudia, na watu hawa. Nafikiri Shreveport inawiwa sana kwa watu kama Jack Moore na watu hawa kama hawa hapa. Juhudi isiyolegea na isiyo na ubinafsi, wamejaribu kujenga mahali ambapo Nuru ya Mungu na Uhai wa Mungu, unaweza kuwaendea watu ambao ni wanaume na wanawake wanaosafiri, ambao wataingia na kufurahia ibada. Naomba lisimame daima, hata kuja kwa Bwana Yesu, mpaka Yeye atakapomaliza nalo.

4 Nami nimefurahia sana makusanyiko, kuitika kwenu kwema kwa hu—huduma, kwa Jumbe. Na mambo makuu ambayo Mungu ametutendea, ni mengi mno. Na hatutajua yaliyomaanisha hadi tutakapovuka upande ule mwingine, kwa sababu mbegu imepandwa ambayo itachipuka katika siku za usoni. Na wengi wameponywa, labda wakati huu hawajui chochote kuuhusu, baada ya kitambo kidogo mtagundua kuwa umetoweka. Na tunaona hayo sana, si tu yale mnayoona yakitendeka; kamwe hamjui yanayoenda kutendeka, yatakayotendeka, kutokana na hayo. Pia ninatumaini kwamba ha—hakutakuwako na watu wowote wanyonge watakaotoka

kwenye mkutano huu, ila kwamba watakuwa na imani ya kutosha kujua kwamba kazi imefanywa, na watakuwa wazima.

5 Kwa wale waliomwinulia Kristo mikono yao, kwa ajili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, na mambo mengi, na ka—kazi za neema mlizohitaji Mungu azifanye pamoja nanyi, ninatumaini tu kwamba kila mmoja wenu atajazwa na Roho Mtakatifu, kila mmoja. Msisahau Ujumbe wangu, juu ya, *Ile Ishara*. Hamna budi kudumu nao. Kumbukeni, ionyeshe Ishara.

6 Sasa inatubidi kuondoka mara moja kwenda Arizona, na Yuma, na Phoenix. Halafu basi tutarudi kupitia hapa Kusini. Sijui tu ratiba ya safari, kwamba ikoje. Lakini tutakuwa hapa, nafikiri, ni huko Louisiana ya chini tena, karibu yapata Februari, mahali fulani hapa katika Louisiana, na Dallas. Na moja kwa moja kuingia, huko Georgia, chini kuingia kwenye huo huko, na kisha kwenda Florida. Ndipo basi tunapaswa kwenda Ulaya kutoka huko, hadi Juni. Ndipo basi tunarudi hapa, kupitia Julai na hadi katikati ya Agosti. Na kisha kurudi, chini kabisa chini ya ardhi, huko Marekani ya Kusini. . . si Marekani ya Kusini, Afrika Kusini. Ndipo kwenye siku ya pili ya Septemba, mwaka huu unaokuja wa 1964, Bwana akipenda, tunaanzia huko—huko Durban, Afrika Kusini, ambapo tuliwaona watu elfu thelathini wakimjia Bwana, kwa wakati mmoja. Ndugu Julius Stadsklev anayeketi hapa, alikuwa mkutanoni wakati huo. Nafikiri hiyo ni kweli.

7 Nami nadhani Ndugu Julius alikuwa ametambulishwa, mtu yule aliyeandika kitabu cha *Nabii Azuru Afrika Kusini*. Nime. . . Dada Stadsklev, hapana shaka, yupo hapa mahali fulani. Si—siwezi kumwona ninii tu. . . naam, ndiyo, sasa ninamwona, pamoja na wa—watoto. Ninakumbuka, miaka michache iliyopita, huko Minneapolis, walikuwa ni jamaa wadogo sana; sasa inanibidi kuwaangalilia juu, wao ni mvulana mkubwa mnene na msichana.

8 Dada Stadsklev hapa, si muda mrefu uliopita, aliyeufanya moyo wangu kuzunguka kweli, mama mdogo, alipoteza mtoto wake mchanga. Naye Bwana alikuwa. . . aliona vema kumchukua. Na yeye alikuwa ameniita, naye alitaka. . . Walikuwa wanaenda kunipeleka Ujerumani kwa ndege. Naye daktari alikuwa mwema sana kungojea, akamwacha mtoto alale hapo. Jamaa huyo mdogo alikufa ghafla, msichana mdogo, mzuri na mnene. Naye Dada Stadsklev alikuwa amempoteza mama yake, na alikuwa amehuzunika sana. Mtoto huyu mchanga bila shaka alikuwa amemhuzunisha sana. Basi akachukua simu, mbali sana kutoka Ujerumani, naye alitaka kuja kwa ndege. Ndipo nikasema, "Dada Stadsklev. . . "

9 Akakiri imani yake, kwamba aliamini kwamba Bwana Yesu alikuwa amenituma kwa ajili ya kazi katika siku za mwisho, na ushuhuda mwaminifu kabisa ambao hakuna mwingine

angaliweza kutoa, naye aliumaanisha kwa moyo wake wote. Alikuwa amemwona Bwana Mungu akifanya mambo kama hayo, akiwafufua wafu baada ya wao kufa. Bali, unaona, wewe kwa kweli, kadiri ninavyo . . . Jinsi, ni utukufu namna gani huo ungekuwa kwa Mungu, huko Ujerumani na kadhalika! Kama ningeweza kulifanya, mwenyewe, ningelifanya. Bali, kitu cha kwanza, hatupaswi kwenda mpaka tujue kile tunachoendea.

10 Kwa hiyo nikatoka nje na kuomba. Nami nafikiri alikaa kwenye simu sehemu ya wakati huo, usiku kucha. Basi kesho yake nikaja, hakukuwa na kitu. Tena Meda akasema, mke wangu, kasema, "Dada Stadsklev alipiga simu mara mbili. Neno lolote kutoka kwa Bwana hadi sasa?"

Nikasema, "Hakuna lolote." Ndipo nikasema . . .

11 Vema, nikatoka nje, nikaomba tena. Nilikuwa mwituni usiku huo. Basi, bila shaka, mtoto huyo mchanga ilibidi ashughulikiwe. Ndipo basi nilipokuwa tu nikiingia, Bwana Yesu, ono likaja, amesimama mbele yangu. Ndipo nikasikia sauti Yake ikisema, "Usikemee huo. Huo ni mkono wa Bwana." Kwa hiyo nikajua basi kwamba Mungu, kwa sababu fulani, alikuwa amempeleka mtoto wake Utukufuni, na hakika ilikuwa ni kinyume na mapenzi ya Bwana kwangu kusema chochote kinyume chake.

12 Ndipo basi nikawazia, "Vema, hilo litakuwa ni sikitiko kubwa. Bali jambo moja nililotenda, nilimjali Bwana. Nilifanya kile Yeye alichoniambia."

13 Hapa si muda mrefu uliopita, nilipokea barua kutoka kwa mhudumu mmoja huko, naye alikuwa ametoa matamshi kwa wahudumu wengine zaidi. Alisema, "Yule . . . " Na yeye alikuwa, nafikiri, huenda alikuwa ni Mjerumani Mlutheri. Sina hakika. Bali alisema, "Kuna jambo moja niwezalo kutamani kwa Ndugu Branham. Wakati msisimko wote ulipokuwa ukiendelea, alikaa imara mpaka akapata uamuzi dhahiri kutoka kwa Mungu, ndipo akajua alichokuwa akifanya."

14 Na hiyo ndiyo njia pekee uwezayo kufanya mambo hayo, ni kusikia kutoka kwa Bwana kwanza, wakati Yeye akinena. Ikiwa angeniambia, usiku wa leo, kwamba niende huko juu na kufufua kutoka kwenye makaburi yale, Rais Kennedy, ningealika ulimwengu mzima uje, uone likifanywa, kwa kuwa ningekuwa na BWANA ASEMA HIVI. Mnaona? Sasa, lakini ninawezaje kusema, "BWANA ASEMA HIVI," mpaka Bwana awe amesema hivyo? Mnaona? Mnaona?

15 Mara nyingi, watu husisimkwa sana na kuingia chini ya dhana na kadhalika namna hiyo, na kile wawezacho kufikiria kwa uwezo wao wa akili. Hiyo si kweli siku zote. Ngojea mpaka Yeye akwambie, nawe unalijua, ndipo umepata hakika. Haikubidi kudhania juu ya hilo. Yeye amekuambia, ni BWANA ASEMA HIVI. Basi Yeye amekwambia, ndipo unaweza kwenda

useme kile Yeye alichosema. Hadi wakati huo, unaweza kwenda na kufanya yote uwezayo, fanya uwezayo mwenyewe, bali huwezi kuwa na hakika mpaka Mungu awe amesema hivyo. Ndipo una hakika.

16 Kwenye kanda ya *Ni Wakati Gani, Mabwana?* Wengi wenu mnayo kanda hiyo, mnaona. Ningeweza kuzungumza kwa ajili ya Matawi na kila mahali pengine, na kusema, "Ni BWANA ASEMA HIVI. Nitakutana na Malaika saba. Na itajulikana, kote katika nchi mbalimbali, mnaona. Na jambo fulani linakaribia kutukia, kwa sababu Yeye aliniambia." Hilo hapo, mnaona, miezi mitatu tu baadaye. Mnaona? Na mambo haya mengine yote, wakati wewe... Wakati Bwana amelinena, halina budi kutendeka.

17 Hiyo ndiyo sababu ninajua kwamba Neno Lake ni kamilifu. Haijalishi kile watu wanawazia kuhusu Hilo, Hilo ni Neno la Mungu. [Ndugu Branham anaipigapiga Biblia yake—Mh.] *Hiyo* ni kweli, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Mnaona, hiyo ni, nasi tunajua ya kwamba hiyo ni kweli.

18 Yesu yuaja. Lini? Sijui. Umbo gani, jinsi atakavyokuja? Nina wazo, bali si—sijui. Imeandikwa *Hapa* ndani, Yeye alisema, "Mimi, nikitwaliwa juu," Yeye angewavuta watu wote Kwake, na Yeye angerudi tena. Ninajua Yeye yuaja. Loo, hiyo ni hakika. Na haijalishi kwangu kwamba ni lini. Mnaona? Kama ni usiku wa leo, ama kama ni mwaka ujao, ama kama ni miaka elfu moja kuanzia sasa, kwamba tu Yeye aje! Nina Uzima wa Milele. Sitakuwa mzee zaidi, nitakuwapo tu wakati Yeye ajapo. Hivyo tu. Hiyo ni, unaona, haijalishi kwangu kwamba ni lini, vipi, ni kwa njia gani Yeye anatimiza hilo, kwamba tu niwe pale!

19 Na Yeye aliniahidi kwamba nitakuwapo, na Yeye tayari amenipa Uzima wa Milele, maana Yeye alisema, "Yeye awezaye kuyapokea Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele; wala hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Hilo ni zuri vya kutosha kwangu mimi. Papo hapo, hilo ndilo yakini yangu. Hilo ndilo yakini yangu. Yeye aliliahidi. Hakuna njia kwa hilo kuweza kushindwa. Kamwe haliwezi kushindwa, si zaidi ya vile Mungu awezavyo kushindwa. Na haiwezekani kwa Mungu kushindwa. Hilo ni jambo moja asiloweza kufanya Mungu, kushindwa. Yeye hawezi kushindwa. Hivi hamna furaha kwa ajili ya hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Loo, jamani!

20 Ninapoanza kuona miaka ikihesabika, na—na kuanza kuona ibada mbili ama tatu kwa siku, zinaanza kunifanya kidogo kuwa mchovu, ambapo hazikuwa zikinisumbua. Lakini basi nafikiri, "Vema, inaleta tofauti gani?"

21 Ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Sisi ni jamaa wa nyumbani tu, kwa hiyo ninataka kuwauliza. Vipi kama una umri wa miaka themanini usiku wa leo, ama una umri wa miaka kumi

na mitano usiku wa leo? Kama una umri wa miaka themanini, na uishi mpaka wakati huu kesho usiku, utaishi zaidi ya watoto wengi, wengi mno wa miaka kumi na sita. Je! uliwahi kuwazia hilo? Hakika utawazidi. Upo hapa kwa kusudi, kumtumikia Mungu. Kwa hiyo ni tofauti gani, umri ulio kwako? Mtumikie tu Mungu.

22 Ikiwa Mungu angenijia na kusema, "Ninataka uende duniani," na—nami nilikuwa huko juu na Yeye akasema, "nenda duniani, nitakupa nafasi ya miaka mia moja ya maarifa, bali ninataka ujichagulie mi—miaka yako. Ni miaka ipi unayotaka kuchukua, ishirini na mitano ya kwanza, ishirini na mitano ya pili, ishirini na mitano ya tatu, ama ishirini na mitano ya mwisho?"

23 Ningesema nini? Vema, kama nitaweka wakati wangu hapa kuwa, loo, mcheza kandanda ama mwanariadha, au kitu fulani, heri nichukue miaka ishirini na mitano ya kwanza. Kama nitakuwa hapa ili kuwa seremala, ama mtu fulani namna hiyo, vema, heri nichukue ishirini na mitano ya pili. Lakini kama ninataka kuchukua kumtumikia Bwana, nitachukua ishirini na mitano ya mwisho, kuanzia sabini na mitano hadi mia moja, kwa sababu, nimekusanya kiasi hicho cha maarifa, ninajua zaidi kuihusu. Mnaona? Mradi tu ninaweza kusimama kwa miguu yangu miwili na kutembea huku, inaleta tofauti gani umri nilio nao? Nipo hapa kumtumikia Bwana, na ni hayo tu. Amina. Hilo lafaa vya kutosha kwangu. Yeye aliliahidi.

24 Sasa ninataka kumshukuru kila mmoja wenu, kwa wema wenu. Na nikitumaini kwamba, Bwana akipenda, kwamba—kwamba tena tutakutana mahali fulani katika ulimwengu huu; kama si tena hapa, tutakutana upande ule mwingine. Na Bwana abariki. Nami ninataka kuomba juu ya leso hizi. Punde tu tutakapoingia kwenye Ujumbe, hatujui kwa hakika kile kitakachotukia. Tulijaribu kuweka usiku kadhaa kwenye. . . tatu, yapata siku tatu usiku; kati ya hizo tano ama sita, siku tano usiku, naamini, Bwana alitupa mwito miongoni mwa watu, wa kuwaita watu watoke, ambapo Bwana angewaponya. Ndipo basi tulikuwa na usiku mmoja, usiku wa jana, tulimleta kila mtu aliyetaka kuombewa, moja kwa moja kupitia mstari wa maombi na kuwaombea. Na nimetumaini kwamba sijashindwa mahali popote kujaribu kufanya yote nijuayo kufanya, ili tuweze kuwa katika hali bora zaidi ya kiroho, na hali ya kimwili, usiku wa leo, kuliko tulivyokuwa tulipoingia hapa yapata siku nne ama tano usiku zilizopita. Nikikosea, Mungu anisamehe, nanyi mnisamehe.

25 Sasa kwa ajili ya Ujumbe wa kufunga, nami nitajaribu kuuweka upesi iwezekanavyo, kwa sababu mimi—mimi huhubiri kirefu. Na nimeliambia kusanyiko langu, na kadhalika, kwamba, kuanzia tarehe mosi mwakani, nitajaribu. Nimeijaribu

kwa miaka thelathini na mitano iliyopita, tangu nilipoingia hudumani, kupunguza kutoka kwa saa hizi mbili, na kadhalika, hadi dakika thelathini. Bali, mimi ni mwenda pole sana, siwezi kusema yale ninayotaka kusema, katika dakika thelathini, ndilo jambo la pekee. Mimi ni wa Kusini, mwajua, na kwa hiyo i—inanibidi tu kuwa hivyo. Siwezi kuliwazia upesi sana. Inanibidi tu kungojea na kuona. Sina budi kumngojea Yeye, kwa ajili ya maneno yangu. Kwa hiyo, lakini mimi—mimi. . .mradi tu ninaweza kumngojea Yeye, nanyi mtavumiliana tu nami.

26 Sasa hebu tusome Maandiko fulani, kwa hiyo tunajua kwamba haya hayatapita. Basi baada ya kuwa na mkutano wetu mdogo wa kukutanika kwa urafiki na kuzungumza, kabla hatujaikaribia sehemu hii ya ibada yenye kicho sana, kuleta Mkate wa Uzima, hebu na tuombe tu kwa mara nyingine.

27 Bwana Yesu, sasa tuna shukrani Kwako. Sote tunakugeukia Wewe, kukushukuru Wewe kwa ajili ya siku hizi kuu na usiku za ibada, kushiriki kwenye Neno, na pamoja na watu. Tunashukuru, Bwana. Roho zetu zimeinuliwa, nasi tunashukuru sana kwamba tumeweza kuketi katika mahali pa Kimbinguni pamoja na Wewe. Na sasa, Baba, kwenye usiku huu mkuu na wa mwisho wa ka—karamu ya upendo, naomba Wewe usimame katikati yetu, tena usiku wa leo, na kuita, "Yeye aliye na kiu, njoo Kwangu." Tujalie, Bwana. Tunajua utatujalia, kwa sababu Wewe hufanya hivyo. Hiyo ndiyo njia Yako ya kufanya mambo, wala Wewe huibadilishi. Nami ninaomba, Mungu, kwamba Wewe utaumega Mkate wa Uzima, kwetu sisi. Jalia tuweze kulipokea Neno hilo ndani ya moyo wetu, litakalotufungulia sote chemichemi ya baraka. Bariki kusomwa kwa Neno, na unisaidie ninapojaribu kuumega Mkate wa Uzima, kwa kusanyiko, kwa haja yoyote iliyopo. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

28 Hebu tugeukie Ki—Kitabu cha Waamuzi, Waamuzi wa Israeli. Na ninataka kugeukia mlango wa 16 wa Waamuzi, kusoma sehemu ya—ya Neno. Waamuzi, mlango wa 16, na ninataka kusoma vifungu vya 27 na 28.

> *Basi nyumba ile ilikuwa imejaa watu waume kwa wake; wakuu wote wa* Wafilisti—*Wafilisti walikuwamo humo, na juu ya dari palikuwa na watu elfu tatu waume kwa wake waliokuwa* wakitazama—*wakitazama, wakati Samsoni alipocheza.*
>
> *Samsoni akamwita* BWANA, *akasema, Ee Bwana* MUNGU, *unikumbuke, nakuomba, ukanitie nguvu, nakuomba, mara hii tu, Ee* Bwana, *ili nipate kujilipiza kisasi juu ya Wafilisti kwa ajili ya macho yangu mawili.*

29 Ni tamasha ya kuhuzunisha jinsi gani! Na somo hili dogo, ninaenda kuchukua fungu kutoka kwalo, kuliita: *Mara Moja Tu Zaidi, Bwana*. Mara moja tu zaidi!

30 Hapana shaka ilikuwa ni siku yenye joto. Walikuwa wamekuwa na sherehe kubwa. Na inanifanya nijisikie vibaya, kila wakati ninapowazia kuihusu, kwa sababu ya aina ya sherehe hiyo ya kidini. Mnajua, sherehe ni sawa, bali ni kulingana na aina ya sherehe hiyo. Na hii ilikuwa ni sherehe moja ambayo kwa kweli ninachukia kurejea. Ilikuwa katika nchi ya Wafilisti. Nao walikuwa wanasherehekea, inanifanya tu kujisikia vibaya kuitaja, "ushindi dhidi ya watumishi wa Mungu." Mtumishi wa Mungu asiye mtiifu alikuwa ameleta fedheha juu ya Jina la Bwana, na akaanguka katika kushindwa, na hawa Wafilisti walikuwa wakisherehekea wa—wakati mzuri wa ushindi, kwamba "samaki mungu wao alikuwa amepata ushindi dhidi ya mtumishi wa Yehova."

31 Kama hilo silo fungu la kumalizia mkutano! Lakini nilijihisi kuongozwa, nilipokuwa nikiangalia kupitia mafungu mia tano au mia sita niliyokuwa nayo pale. Macho yangu yakaangukia fungu hili hapa, nami nikawaza, "Ninaamini nitazungumzia hilo kidogo tu usiku wa leo." Na labda hilo ndilo Roho Mtakatifu angetaka tujue jambo kulihusu hapa ndani. Ninii . . . kuhusu . . .

32 Siku yenye joto, naamini, nazo kafara zilikuwa zinateketea katika moto karibu na huyu samaki mungu mkuu, na kulikuwa na Wafilisti elfu tatu wakiwatazama hao wawili walipokuwa wakiingia kwenye uwanja huo mkubwa wa michezo. Hapana budi ulikuwa ni kama uyoga, jinsi walivyoutengeneza. Kama vile, ningesema, kitu katika mfano wa—wa uyoga ama kiyoga, kilichopinduliwa namna *hii*, kikiwa na nguzo chomozi mbili kubwa, ama—ama miimo, ikishikilia uwanja wa michezo, ukionekana zaidi wenye umbo *hili*, labda, ili watu kwenye uwanja huu mkubwa wa michezo wangeweza kuangalia chini kutazama tafrija iliyokuwa ikiendelea katika sakafu kuu.

33 Na majemadari wakuu wa vita wenye ustaarabu mkubwa walihudhuria mkutano huo, na wanawake wao waliojipamba kwelikweli walikuwepo mkutanoni. Ndipo wote wakasimama ghafla, kuinama, tafrija kuu ilikuwa karibu kuanza. Tunakuwa wakati mwingine, na kile tunachokiita, kitangulizi, wao . . . ndipo basi kianzishi, kitangulizi cha ta—tafrija yenyewe. Nao walikuwa wamekuwa na burudani nyingi, kama walivyofanya wakati mwingine, kutoa kafara na kuua, na kadhalika. Lakini sasa ta—tafrija yenyewe ilikuwa tu karibu kuanza, na kundi hili lote la watu mashuhuri, wa ninii yote . . . wa maeneo katika nchi ya Wafilisti. Walisimama, kwa sababu walikuwa ma—matajiri. Walikuwa wameketi juu, katika hii ninii kubwa, tungeuita, kama uyoga. Na labda maskini, na kadhalika, walikuwa hapa chini kwenye—kwenye sakafu. Bali wao waliketi juu mahali wangeweza kutazama vizuri, na kuona tafrija yote. Kilikuwa ni—kilikuwa ni kibanda cha watu mashuhuri. Elfu tatu ya hao! Hewa ilikuwa imejaa harufu ya pombe, makelele na vifijo vya ulevi siku nzima, wakinywa pombe na kudorora, na kufanya

yasiyofaa, jinsi ghasia za ulevi ziwezavyo kuwa hivyo. Basi wote wakasimama, kwa sababu ta—tafrija kuu ilikuwa karibu kuanza, nao wakainama. Walitaka kupata mtazamo mzuri. Wasingeweza kukosa hii, kwa kuwa hii ilikuwa ndiyo tafrija yenyewe.

34 Waliona nini? Mvulana mdogo akimwongoza mtu aliye kipofu hadi katikati ya uwanja, kwenye karamu ya mungu samaki, Dagon. Mvulana huyo aliliongoza hili lundo la nyama kipofu, linalojikwaa, kipofu, hadi kwenye mwimo, na kumsimamisha kando ya mwimo, kufanya tafrija.

35 Kwa hiyo huyu ni Samsoni, mtu ambaye alikuwa m—mtumishi mashuhuri wa Mungu, sasa anasimama hapo, amefedheheka, kipofu, mnyonge, aibu. Ni picha ya ki—kizazi kilichopotoka, kilichodididimia. Ni picha ya—ya ta—ya taifa ambalo limepoteza msimamo wake na Mungu. Ni picha ya kanisa lililopoteza msimamo wake kwenye Neno la Mungu, maana hilo ndilo Samsoni alilowakilisha hapa. Amefedheheka, akavunjika, alikuwa katika hali mbaya alipokuwa ameketi pale, ama kusimama pale, hasa. Kwa hiyo ungeweza kumwazia akiwa amesimama, mtu huyu mashuhuri ambaye, wakati mmoja, yale aliyoweza kufanya; naye huyu hapa amesimama hapa katika hali hiyo, amefedheheshwa, kama nilivyosema, amevunjika, mfano ambao ninataka kutangaza usiku wa leo. Mfano huu unawakilisha saa yenyewe tunayoishi, hali ya kanisa sasa; limevunjika, nje ya Neno la Bwana; limefedheheka, nje ya mahali pake. Nalo swali linakuja, leo hii, mkono umeandika ukutani na ni nani awezaye kuyasoma? Hawajui lolote kuyahusu.

36 Hebu tuchukue na kuchunguza nia za wale Wafilisti. Jina lenyewe la mtu huyu, Samsoni, wakati mmoja, lilifanya taifa lote kutetemeka, kutaja tu Samsoni, maana Mungu alikuwa pamoja naye. Nayo mataifa yalitetemeka kwa sababu ya jina lake lenyewe.

37 Hivyo ndivyo ilivyokuwa, Jina la Yesu Kristo, lakini sasa linatumika kama neno la matusi, mzaha. Hakuonekani kuwa na heshima yoyote Kwalo. Wakati, hilo Jina linapita kila jina lililowahi kutamkwa katika vinywa vya wanadamu. Ni Jina ambalo hata limeinuliwa sana juu ya kila jina lililoko Mbinguni, kila jina duniani, na familia yote huko Mbinguni na duniani inaitwa Jina Hilo. Na hata hivyo wanadamu wanachukua Hilo katika maneno ya matusi, washiriki wa kanisa wanalitumia Hilo katika mizaha, na viongozi wengi wa kidini hulikufuru Hilo kwa kanuni zao za imani. Hiyo ndiyo sababu kwamba tumeaibika, mbele ya ukomunisti, Urumi, na Uprotestanti, na mambo yanayoinuka duniani leo hii. Na hiyo ndiyo sababu kwamba tumeaibika. Tunapaswa kujua majibu haya. Mungu

anayo katika Kitabu Chake, kwa ajili ya siku hii, bali tumeendea kitu kingine, tukasahau Hicho.

38 Wengi wa hawa Wafilisti, waliposimama pale, kati ya hao askari wakuu wa vita, hapana shaka . . . Mtu fulani alitangaza, kwamba, "Tukio linalofuata ni Samsoni." Wengi wa hao askari wa vita, pamoja na wake wao wazuri waliojipamba kwelikweli, waliangalia kwenye uzio na kukumbuka kumwona Samsoni akisimama kwa njia tofauti, wakati mmoja wakati Roho wa Bwana alipokuwa juu yake; akisimama ameshika mfupa wa taya la nyumbu, mikononi mwake, huku Wafilisti elfu moja wamelala kando yake. Nao walikuwa wamekimbilia kwenye mwamba mahali fulani, kutafuta usalama.

39 Wakati mtu alipochukua mfupa wa taya la nyumbu uliokuwa umekaa huko jangwani, yeyote anajua kwamba huo ukigongeshwa kwenye mwamba ama chochote, na mfupa huo, ungevunjika vipandevipande. Na zile helmeti, baadhi yake zilikuwa inchi moja, hadi inchi moja na nusu, unene, wa shaba. Naye mtu huyu hakuwa askari wa vita, wala hakuwa mtu aliyefunzwa ku—kutumia mkuki. Nao Wafilisti wakiwa na koti la deraya, deraya iliyofungwa ukanda, umepita kama dirisha la luva, pamoja na chuma kinachozuia mikuki na kadhalika zisiwagonge; na pia pamoja na helmeti, na pamoja na ngao, na pamoja na mikuki. Nao wakamzunguka mtu huyu, Samsoni, na kuwazia, "Walio bora zaidi kwenye jeshi wataweza kumchukua mtu huyu."

40 Naye hakuwa na kitu mkononi mwake. Ndipo akapata mfupa wa kale mkavu wa taya la nyumbu, na akaanza kugonga, kulia na kushoto, mpaka akawaangusha Wafilisti elfu moja. Kwa nini? Biblia ilisema, "Roho wa Bwana alikuwa juu yake."

41 Hapa akasimama, tofauti sasa. Alikuwa ametoa siri yake. Na wao waliweza kumkumbuka vizuri kabisa.

42 Huenda kulikuwa na kundi jingine pale juu, wangeweza kukumbuka usiku mmoja wakati Delila alikuwa amemroga akamwingiza kwenye—kwenye mji wa—wa Gaza. Nao walikuwa wamefunga malango yao makubwa, labda yenye uzito wa tani moja ama zaidi, kila moja, malango makubwa ya shaba ya mji, yaliyokuwa na nondo za chuma zilizoingia chini kwenye miamba na kufungwa, yakiwa na bawaba hivi kwamba hata tusingeweza kuwa na kama hizo leo hii. Ndipo wakasema, "Wafilisti wanakujia, Samsoni." Na wengi wa askari wa vita waliosimama karibu na lango, hata wasiweze kuongea, wakati alipoweza kuvunja hizo nyugwe na kuondoka akitembea. Nao walitawanyika kama kundi la mende wakati wa usiku, wakati taa imewashwa. Roho wa Bwana juu yake, alinyosha mkono akang'oa lango moja, kisha akang'oa hilo jingine, akayatia begani mwake na kutembea akikwea kilima, kisha akaketi. Waliweza kukumbuka hayo. "Ni askari wa vita kiasi gani,"

wengi wao wangeweza kukumbuka hayo, ya kumwona katika ushindi mkuu, "bali hebu mwangalie sasa!"

43 Hiyo ndiyo picha ya kanisa. Ninaweza kusoma kwenye Biblia, kuhusu kanisa wakati lilipojazwa na Roho Mtakatifu kwa mara ya kwanza, ishara kubwa na maajabu yaliambatana na mkutano wao. Tunaweza kukumbuka miaka michache iliyopita, miaka arobaini au hamsini iliyopita, wakati kanisa lilipojazwa na Nguvu zizo hizo. Bali liangalie leo hii, linasimama limevuliwa nguo. Kitu fulani kimelivua nguo, kitu kile kile kilichomvua Samsoni, yote yalisababishwa na kumsikiliza mwanamke aliyemweka ndani. Na ni kitu gani kilicholivua nguo kanisa, ni kusikiliza hali hiyo ya mwanamke aliyeundiwa dhehebu, yule Yezebeli wa kale. Kitu kile kile ambacho Samsoni aliinuliwa aweze kukishinda, kilikuwa kimemshinda. Nalo kanisa la Pentekoste, usiku wa leo, linasimama katika mikondo iyo hiyo. Kitu kile kile lilichoinuliwa kushinda, udhehebu, limejiunganisha likarudi ndani yake tena, na nguvu zake zimetoweka. Kweli. Nguvu za Bwana zililiacha.

44 Tulipaswa kujua kwamba kila wakati, kote katika historia, ambapo kanisa liliwahi kujiundia dhehebu, Mungu aliliacha papo hapo. Lilianguka na kamwe halikuinuka tena. Na Pentekoste ilikuwa ni kitu kilichotoka katika dhehebu, bali, kile kilichokuwapo, tulichukua uongozi wa binadamu badala ya Roho Mtakatifu.

45 Na hilo hasa ndilo Samsoni alilofanya. Wazia hilo, kile ambacho hapana shaka kilimpitikia mtu huyo akilini wakati aliposimama pale. Hapana budi aliwaza kuhusu ushindi wote mkuu ambao Mungu alikuwa amempa, mambo makuu ambayo Mungu alikuwa amefanya pamoja naye na kwa ajili yake; na jinsi ambavyo, wakati alipokuwa pamoja na Mungu, nguvu za Roho Wake, na furaha na amani aliyokuwa nayo wakati alipokuwa pamoja na Mungu, na ya Mungu na watu Wake. Jinsi ambavyo Samsoni alikuwa amempungukia! Sasa, taifa lile lile ambalo Samsoni aliinuliwa kuangamiza, lilikuwa limemfunga.

46 Nacho kitu kile kile ambacho Mungu aliinua Pentekoste kufanya, kimewafunga, kikawavua ushirika, kikawavua nguvu; kugombana, kukasirikiana, washiriki vuguvugu. Mambo mazuri, makubwa, kila kitu, lakini wangekuwa afadhali kama wangeninii—kama wangekuwa na ngoma ya kale ya Jeshi la Wokovu, ama maskini gitaa la kale, huko chini pembeni mahali fulani tena. Afadhali niwe nayo namna hiyo, kuliko kuwa na makanisa yetu makuu ya dayosisi tunayopata, yenye thamani ya mamilioni ya dola.

47 Lakini huyo akasimama pale. Alikuwa ameshindwa. Sasa alikuwa ni mfungwa wa taifa lile lile ambalo Mungu alimwinua kuangamiza.

48 Walikuwa naye akifanya vitimbi, kuwatumbuiza. Na hayo ndiyo yote yaliyoko leo hii, namna fulani ya vitimbi kidogo ili kujaribu kuwatumbuiza.

49 Kumwacha mwanamke amshawishi kutoka kwa Neno la Mungu lililoahidiwa! Hilo ndilo jambo lile lile kanisa lililofanya, limemwacha mwanamke, Yezebeli, "mama wa makahaba," aliyewakilishwa katika Ufunuo 17, kuwashawishi moja kwa moja kurudi katika matapiko waliyotoka ndani yake. Kama Biblia isemavyo, "Kama nguruwe aendavyo, kurudi kwenye kugaagaa kwake, na mbwa kwenye matapiko yake."

50 Na mradi tu huyo nguruwe anabaki kuwa nguruwe, ataninii, asili yake ni nguruwe, atarudi moja kwa moja kwenye kugaagaa. Na, wewe, njia ya pekee ya kumweka nje ya shimo la matope ni kubadilisha asili yake.

51 Hiyo ndiyo njia ya pekee unayoenda kupata tofauti yoyote kanisani leo hii, halina budi kuwa na badiliko la asili. Na badala ya mfumo fulani wa kikanisa kuwaongoza wahubiri huku na huku, itahitaji Roho Mtakatifu, kupitia Neno, kuwaongoza kuwarudisha kwenye ile roho ya kumcha Mungu tena. Hiyo ni kweli. Kama mbwa alitapika na yalimchefua katika tumbo lake, mara ya kwanza, si yatamchefua tena? Na kama Mungu alituita kutoka kwenye mchafuko kama huo, kwa sababu. . . vema, si itafanya jambo lile lile tena? Halafu tunarudi moja kwa moja ndani yake, kitu kile kile. Haipaswi kufanywa.

52 Mfumo huu wa Yezebeli, sasa kipofu kiroho, ninasema, kwa Neno la Mungu, wakijiunganisha moja kwa moja kwenye Baraza la Makanisa. Kila kitu, fundisho letu kuu la kiinjilisti, inatubidi kuacha hilo, ili kuwa dhehebu. Maana, madhehebu yote ambayo hayako katika Baraza hili la Makanisa, ninayo karatasi juu ya hilo, kwamba hata kama kanisa lako haliko kwenye Baraza hili la Makanisa, katika wakati wa shida, wanaweza kutumia kanisa lenu kuweka zana za vita au chochote watakacho. Na iwapo mtu yeyote atashikwa akimwombea mtu yeyote, nje ya kushirikishwa na Baraza hili la Makanisa, anaweza kupigwa risasi, kama kosa dhidi ya serikali ya shirikisho. Hiyo ni kweli. Ninayo makaratasi juu yake, kutoka Washington. Ninyi, wanaenda kuwalazimisha kuingia katika hilo. Hiyo ndiyo sababu nimekuwa nikipinga mfumo huu wa kidhehebu. Ndiyo hiyo. Ilinibidi kunyamaza kuhusu huo kuwa ndio alama ya mnyama, bali wakati umeenda vya kutosha hata mnaweza kujua kuwa ni kweli. A-ha. Mnaona? Ni kweli. Ni hivyo hasa.

53 Sasa umefanya nini? Umelileta kanisa, ukalivua nguvu zake, si kitu ila jina, inaonyesha picha yake hasa katika Ufunuo 3, Wakati wa Kanisa la Laodikia, wamemkataa Kristo, naye yuko nje. Hakika. Kwa nini? Lilifanya hasa kama mama yake alivyofanya, likarudi kuwa dhehebu. Pentekoste, ilizaliwa nje ya madhehebu, ilizaliwa nje ya hayo; na punde tu walipopata

kundi la watoto kuja kutoka kwenye shule fulani, na iliwabidi kuwa na seminari na kadhalika, badala ya vyumba vya juu. Na sasa, mengi ya makanisa hayo makubwa, mtu lazima apite uchunguzi wa mtaalamu wa magonjwa ya akili kabla hajaruhusiwa kuwa mmishenari katika nchi za ng'ambo. Kanisa la mwanzoni halikuwabidi kuchunguza, uchunguzi wa mtaalamu wa magonjwa ya akili, bali iliwabidi kupitia uchunguzi wa Damu ya Yesu Kristo, ndiyo iliyoleta tofauti.

54 Angalia, Samsoni alitoa siri yake kwa Delila. Hatimaye alimpenda na kumpapasa, na kumwambia alikuwa ni mtu mzuri, jinsi alivyompenda, mpaka akagundua mahali siri ilipokuwa, ndipo akainyoa na kuiondoa siri hiyo.

55 Na hivyo ndivyo hasa vile maskini mama Yezebeli amelifanyia kanisa la Kiprotestanti, imetokea. Na sasa wanapatana juu ya mafundisho machache madogo waliyosema wanayo, ili waweze kuwa na umoja juu ya ulimwengu. Na mahali pa kwanza kanisa liliponyolewa vishungi vyake palikuwa ni huko Nikea, naye anaenda kuvinyoa tena tangu amekuwa hapa. Hiyo ndiyo siri yake, ni Neno. "Mkikaa ndani Yangu na Neno Langu ndani yenu, mnaweza kuomba lolote mtakalo, mtapewa." Mnaona, hapo ndipo wanapopoteza siri yao. Sasa waangalie, wameshindwa tu kama Samsoni alivyoshindwa. Wahudumu, badala ya kuzaliwa . . .

56 Kama David duPlessis alivyosema wakati mmoja, "Mungu hana wajukuu wa kipentekoste."

57 Lakini hivyo ndivyo unavyosema, "Mama yangu alikuwa ni mpentekoste. Alipata tukio. Alifanya *hili*. Baba yangu alifanya *fulani na fulani*." Hilo halina uhusiano wowote na wewe. Inakubidi kuwa na jambo lile lile.

58 Sasa tunazo seminari ambazo huangua wahudumu wetu, na tunajenga kubwa zaidi kila wakati. Pia—pia tunao wanafunzi wa saikolojia. Na hiyo ni sawa ikiwa unataka kufunza saikolojia, bali mimi sijali kuhusu saikolojia. Ninataka tu kumjua Yesu Kristo, ni hayo tu ni—ni . . . yote nitakayo kujua, ni Yeye. Sasa tunaona kwamba tumelipata. Hakika halina budi kutimiza unabii wa Timotheo wa Pili 3, ambapo wangekuwa, "vuguvugu," mwajua, "wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko Mungu, na wasiotaka kufanya suluhu, wasiotosheka, na—na wakali, na wasiopenda walio wema."

59 Hilo limetufanyia nini? Karibu limefanya wanawake wetu Wapentekoste onyesho la Hollywood. Hiyo ni kweli. Ilikuwa kosa kwenda kwenye sinema, maonyesho. Lakini sasa, mwajua, ibilisi aliwashinda tu kwenye hilo, aliiweka moja kwa moja nyumbani. Mnaona? Hiyo ni kweli. Ilikuwa ni kosa kufanya hivyo. Ilikuwa ni kosa kwa dada zetu kukata nywele zao au kuvaa nguo fupi. Lakini sasa sivyo, sio katika njia ya mawazo ya Kipentekoste, katika dhehebu lao. Bali ingali ni kosa, kwa Neno la Mungu!

Lakini, mnaona, wameondolewa nguvu za—za—za—zao. A-ha. Mnaona? Na kisha wanasema, "Vema, kanisa letu linaamini . . ." Sijali kile kanisa lenu linachoamini. Ni kile Mungu alichosema! Hiyo ndiyo sababu yeye anasimama, leo hii, bila jibu.

60 Hivyo ndivyo hasa Samsoni alivyosimama. Samsoni alikuwa vivyo hivyo. Hapana shaka aliwazia makosa yake, alipokuwa amesimama pale. Siamini mtu angeweza kusimama pale na awazie vizuri, ila yule ambaye angewaza, akijua, ndiye huyu hapa sasa, amekuwa tu ji—ji—jiwe la kujikwaa. Ni hali ya jinsi gani, mtu mkubwa mnene amesimama pale! Uwanaume wote uliowahi kuwa ndani yake, kadiri ya yale ninayoita misuli, kila mmoja ulikuwepo. Bado alikuwa na misuli. Angali alikuwa na misuli mikubwa, misuli yake alikuwa nayo. Alikuwa na ngumi nene kubwa. Alikuwa angali labda ni mkubwa tu kama alivyowahi kuwa. Kwa kweli, kanisa la Kipentekoste ni kubwa zaidi ya lilivyowahi kuwa, lakini Mungu alikuwa wapi? Jambo ndilo hilo. Naam. Alipokuwa amesimama pale, akiyakumbuka makosa yake, alikumbuka kilichoyasababisha kwanza. Kilichoyasababisha, kwanza, hakikuwa hasa macho yake ya kawaida kung'olewa, bali kilikuwa ni kupofushwa macho yake ya kiroho, kwamba alimruhusu Delila amshawishi kumwingiza ndani yake.

61 Na hilo ndilo limelizuia kanisa leo hii, ni, maono ya kiroho ya Neno la Mungu limebadilishwa na lundo la kanuni za imani. Hilo ndilo jicho alilo nalo ibilisi. Jambo la kwanza awezalo kufanya, ni kuyapofusha macho yako, kukuambia, "Ni kundi la watakatifu wanaojibingirisha," kukuambia, "Ni *hili*, *lile*, ama *linginelo*, au kazi fulani ya ibilisi, ama ni kuwasiliana kimawazo, au kitu kama hicho." Kama anaweza kuyang'oa macho yako, uko gizani.

62 Basi angalia ombi la kwanza la Samsoni katika maombi yake, "Bwana, nipate kujilipiza kisasi kwa ajili ya macho yangu mawili!" Alijua hapo ndipo shida yake ilipotokea. Angalia, vishungi vyake vilikuwa vimekua, bali alikuwa kipofu. Ingembidi kuyumbayumba, siku zake zote. Alikuwa kipofu.

63 Tunaweza kuwa na mtambo mkubwa kama tuliowahi kuwa nao, na washiriki wengi hivyo; bali inafaidi nini, kama wewe ni kipofu kwa kitu chenyewe kinachoendelea mbele yako, nawe huwezi kukiona? Kinachotendeka papa hapa, siku baada ya siku, pamoja na watu, Roho Mtakatifu akijifunua Mwenyewe, na watu hawakioni. Huo ni upofu, upofu wa kiroho!

64 Walisimama na kumwangalia Yesu akitenda miujiza, na kadhalika, na kujitangaza Mwenyewe kuwa ni Masihi, nao wasingeweza kuliona. Yeye alisema, "Wana macho, bali hawawezi kuona." Walikuwa vipofu.

65 Naye Samsoni alikuwa kipofu. Lakini hili hapa alilotambua Samsoni, ambalo kanisa halijalifikia bado, alijua kulikuwa na uwezekano wa kurudi tena.

66 Ikiwa kanisa lingeweza tu kujua hilo, uwezekano, lakini watu wa siku hizi inaonekana hawalipati ono bado. Hawaonekani kulipata, kwamba kuna uwezekano. Halitimii. Mnaweza kupaza sauti zaidi kidogo, kupiga makofi zaidi kidogo, au kucheza zaidi kidogo, hilo silo. La. Ni kurudi kwenye Neno; kuna uwezekano wa kurudi na kurudisha Neno ndani tena. Ulilipita pale. Angalia, wanaketi kimya. Loo, hakika, kupiga makofi yao? Naam, bwana. Lakini, unaona, hayo ni maneno matupu, bila chochote.

67 Nimewaona makafiri wakipiga makofi yao, wakicheza, wakinena katika ndimi, na kufanya mambo hayo yote, na kufasiri, bali walikuwa ni makafiri wa Kiafrika. Hakika. Nimewaona wakiweka penseli chini, na huyo mchawi alisimama hapo na kuifanya penseli hiyo kusimama, na kukimbia huku na huku kwenye mahali fulani pale juu, na kurudi na kucheza, kama, "kunyoa na kukata nywele, pesa nane," na kusababisha kuongea lugha zisizojulikana na kuziandika, kisha mmoja wao akasimama pale, akizifasiri. Loo, jamani!

68 Huwezi kutegemea hayo. Wengi wao huzungumza katika ndimi huku wakikana kanuni zenyewe za Yesu Kristo. Nimeichukua Biblia yangu, nikaiweka Hiyo moja kwa moja kwa mtu; yeye akiwa amesimama hapo, akinena katika ndimi. Nami ninasema, "Ndugu, *Hii* ni hakika."

69 "Sitaki hata kuona Hiyo. Utukufu kwa Mungu! Ninajua yale Yesu aliyosema, sijali kuhusu mengine ya Hiyo. Haleluya! Utukufu kwa Mungu," namna hiyo. Mbona, mtu ambaye ataugeuza mgongo wake kwenye Kweli na kwa kweli kufanya ghasia namna hiyo, kuzuia kuiona Kweli, huo ni unafiki, na upeo wake, kwa sababu tu itambidi kusalimisha kadi yake ya ushirika kama akiikubali Kweli. Hiyo ni mbaya kuliko Samsoni. Angalieni, bali hawakushika Hiyo. Wanakaa kimya.

70 Sasa, loo, hakika, tuna mikusanyiko kwa ajili ya tafrija, tunaiita, "mikutano," miamsho ya kilimwengu, na kadhalika, yote imejaa mikogo, hakika, mambo makubwa mashuhuri, na matangazo makubwa ya biashara, "Mtu aliye na ujumbe wa wakati, na *Fulani* na *Fulani*." Tunayo hayo yote, lakini yu wapi Mungu? Hilo, hilo ndilo jambo tunalotafuta, yu wapi Mungu? Onyesho kubwa la usomi, mtu mwenye elimu ya kutosha ambaye asingeninii. . .anatumia neno ambalo nusu ya watu wasingeweza kuelewa kile alichokuwa akisema, na hata hivyo ana digrii ya heshima, na digrii, na digrii, na digrii, hata anaweza kutoa utaratibu wa masomo ya kawaida na kuweka maneno pamoja, na kusimama wima kabisa, na kusema "amina" vizuri

sana, na kugeuka kama mwanajeshi, atembee kutoka jukwaani. Lakini yu wapi Mungu?

71 Samsoni alikuwa amesimama mahali hapo wakati mmoja, mwenyewe, na kujua nguvu za Mungu, bali sasa alikuwa amenyolewa hayo majaliwa. Alikuwa tu mkubwa kama alivyowahi kuwa, lakini Mungu hakuwepo.

72 Tuna mengi ya hayo leo hii. Ni vibaya sana kwamba tunayo, lakini tunayo. Sasa tunaona. Bali hayarudishi Roho wa Mungu. Sasa, jambo ni kwamba, watu hawako tayari kulipa gharama kurudi katika Hilo. Ninaamini kwamba Mungu anabaki tu jinsi Yeye alivyowahi kuwa. Lakini, jambo ni kwamba, watu wamefungamanishwa sana katika ulimwengu, na ulimwengu ndani yao, mpaka wana dini tu ya kutosha kuwafanya wenye mashaka. Si ya kutosha kujiachilia kwa Mungu kweli na kutoa moyo wako wote katika Yeye, bali ya kutosha, "Naam, mimi huenda kanisani. Hakika, ninafurahia uimbaji mzuri na kupiga makofi. Naam, ninapenda hilo, mnaona."

73 Bali inapofikia moja kwa moja kuweka kile unachosema kuwa unaamini katika matendo, na kuwa tayari kukiri makosa, hawafanyi hivyo. Haipo kabisa. Hawana hiyo. Vema, hiyo ni imani halisi. Hiyo ndiyo tunayohitaji. Tuliacha hiyo kitambo, muda mrefu uliopita, na kuibadilisha. Maombi, na—na maungamo, na imani, tuliibadilisha na mhemuko, kutetemeka, ama kutikisika, au kuruka juu-chini. Hiyo ndiyo sababu hakuna kushikilia imara, maana hakuna kitu pale cha kuwashikilia, mpaka uje kwenye msingi wa Neno la Mungu, wa sikitiko la kiungu, tayari kutubu na kusahihisha chochote, na kufanya yaliyo mema, tayari kuishi maisha mema. Sijali yale watu wanayosema, au chochote kile, wewe ishia yako, kwa ajili ya Yesu Kristo na yale aliyosema. Basi ukichukua kanisa kama hilo, kurudi, kuna uwezekano wa hilo kurudi. Lakini hawako tayari kufanya hivyo.

74 Samsoni aliomba sawasawa, "Bwana, jalia nife na hawa Wafilisti." Loo, jamani! Mnaona kinachoenda kumgharimu? Vipi kama Mungu akiyajibu maombi yake? "Jalia nife." Loo! Ninapenda hilo.

75 Je! ni Patrick Henry aliyesema, "Nipe uhuru au unipe mauti"? Hiyo ni kweli.

76 Vema, jambo ndilo hilo, uhuru au mauti! Ni kurudi kwa Mungu, ama—ama kifo. Tunaenda kufanya nini? Tunaiga nini? Ni nini tunajaribu kuigiza, Ukristo? Ikiwa Roho Mtakatifu angali ni Roho Mtakatifu yeye yule aliyeshuka Pentekoste, angali anafanya mambo yale yale aliyofanya wakati ule. Nguvu zile zile, Roho yule yule, atafanya kazi namna ile ile. Hatuhitaji baraza la makanisa. Tunahitaji Biblia kurudi katika matendo. Hiyo ni hakika.

77 Sasa tunaona kwamba Samsoni aliomba sawa, “Bwana, jalia nife pamoja na adui,” kumfia adui aliyekuwa amemweka kwa njia ile. Kama kuna jambo ambalo watu wanapaswa kuombea, usiku wa leo! Nasi tunaona kitu kilichofanya hili, ni kuondoka kwenye Biblia, kwendea kanuni za imani. Basi, kufa na kitu hicho, toka ndani yake! Kufa kwa ajili yake. Samsoni alikuwa tayari kulipa gharama ili kufanya Nguvu za Mungu zirudi tena. Kuna gharama ya kulipwa kwa ajili Yake, bali, leo hii, watu hawaonekani kufanya hivyo.

78 Loo, tunasikia uamsho, hakika. Naam, tuna uamsho wa kimadhehebu, kuingiza wafuasi zaidi, na mambo kama hayo. Lakini yaangalie maadili, daima yanazorota. Angalia jinsi wanavyozidi kwenda mbali na mbali na Mungu kila wakati, wakienda mbali na Neno. Na sasa wakati wanapoingia na kuja kwenye Baraza la Makanisa, mbona, wamemkubali mwuaji mkubwa kuliko wote kanisa liliopata kuwa nao. Neno ambalo Mungu aliwaachia, wanaruka yote ya Hilo. Huwezi kuifundisha Biblia hiyo; inakubidi kufundisha kanuni yao ya imani. Jambo ndilo hilo.

79 Samsoni alijua jambo moja, na sijui kama kanisa linatambua leo hii. Alijua kwamba hali yake ya kurudi nyuma isingeweza kukabiliana na changamoto ya wakati huo. Nami ninajua, leo hii, kwamba hali ya kurudi nyuma kwa kanisa haiwezi kukabiliana na changamoto ya wakati huu. Na itakuwa mbaya zaidi. Biblia ilisema, “Kama Yane na Yambre walivyompinga Musa, ndivyo na wao; watu wenye akili potovu, kuhusu Imani.” Karibu wanaweza kuiga Hiyo kikamilifu.

80 Musa alishuka chini pamoja na amri yake kutoka kwa Mungu, akiwa na fimbo mkononi mwake. Ndipo Mungu akasema, “Fanya ishara *hii* mbele yao. Na iwapo hawatasikiliza hiyo, basi fanya ishara *hii* mbele yao. Na iwapo hawatasikiliza hiyo, basi nitakuwa pamoja nawe, nitashughulikia yaliyosalia.”

81 Vema, Musa alishuka na ishara yake ya kwanza. Ndipo, mara tu alipofanya ishara yake ya kwanza, kulikuwako na waigaji kila mahali, wakifanya jambo lile lile. Lakini Musa hakuhangaika kuhusu hiyo. Alisimama tu kimya, kwa kuwa alijua kwamba Mungu ndiye aliyemtuma. Tunaenda kuwa na hiyo ikijirudia tena katika siku za mwisho, kumbukeni. Mnaona?

82 Nayo hali yetu ya kurudi nyuma sasa haitakabiliana na changamoto ya wakati huu, hata hivyo mwili wote mkubwa upo hapa. Wapo Wapentekoste wengi ulimwenguni leo kuliko walivyowahi kuwapo, tuwajuao, waaminio wengi zaidi Wapentekoste. Hiyo ni kweli.

83 Mnajua, *The Sunday Visitor*, gazeti la Katoliki, gazeti la Jumapili linaloitwa *The Sunday Visitor*, ninaamini yapata miaka miwili iliyopita, lilitoa tamshi fulani namna hii. Alisema, “Kanisa linalokua upesi kuliko yote ulimwenguni

ni Wapentekoste." Kasema, "Mwaka jana, kanisa Katoliki liliandikisha waongofu milioni moja, kwa Ukatoliki." Bali kasema ninii . . . Huo ni Ukatoliki wote. Bali kasema, "Kanisa la Kipentekoste pekee, lenyewe, liliandikisha milioni moja, laki tano."

84 Sasa mwili upo, bali hatuna nguvu tulizokuwa nazo tulipokuwa wachache. Mwili wote mkubwa wa Samsoni ulisimama pale, lakini zilikuwa wapi Nguvu za Bwana? Naam, mfumo wa kimadhehebu hauthibitishi Neno la Bwana. Hiyo ni kweli. Sasa angalia.

85 Nilikuwa nikizungumza na kasisi anayeishi kando ya barabara kutoka kwangu, kanisa la Moyo Mtakatifu.

86 Yapata mwezi mmoja uliopita, tangu toleo hili jipya kutokea, mhubiri wa Kilutheri alimwalika kasisi wa kanisa Katoliki, kanisa la Moyo Mtakatifu, kumhubiria katika mimbara yake. Naye ka—kasisi wa Katoliki akamfanya mhudumu wa Kilutheri kumsomea misa. "Kubadilishana mimbara," taarifa kubwa katika gazeti. Naam. Hakika. Loo, jamani, kama yeyote angeona hilo na asininii . . . Kama huwezi kuelewa hilo, vema, wewe ni—wewe ni—wewe hakika ni kipofu Kimaandiko. Mnaona? Ndiyo.

87 Nilizungumza na kasisi huyu. Naye akaniambia, akasema, "Ninataka kuzungumza nawe, Bwana Branham."

Nikasema, "Vema."

88 Ndipo akasema, "Je! ulimbatiza huyu msichana wa Frazier, jina lake Mary Elisabeth Frazier?"

Nikasema, "Naam, bwana, nilimbatiza."

Akasema, "Askofu anataka taarifa yako iliyotiwa sahihi juu ya hilo."

Nikasema, "Ninasikia kwamba—kwamba alibadilika kuwa Mkatoliki."

89 Naye akasema, "Naam," kasema, "alirudi kwenye kanisa mama."

90 Ndipo nikasema, "Naam, bwana," nikasema, "mama yake alikuwa akiniambia habari zake."

Kasema, "Naam, mama yake hakulichukulia vizuri sana."

91 Nikasema, "Naam, mama yake aliniambia 'ni afadhali aende naye kaburini.'" Nami nikasema, "Kwa kweli, hilo ndilo alilokuwa anafanya."

92 Basi kwa hiyo akasema, akasema, "Ninakutaka utie sahihi taarifa hii." Kasema, "Je! ulimbatiza? Ulimbatiza namna gani?"

Nikasema, "Katika ubatizo wa Kikristo."

93 Naye akasema, "Ninamaanisha *kwa njia gani*, bwana? Je! ulimnyunyizia maji, kummwagilia, au kumtumbukiza?"

Nikasema, "Ubatizo wa Kikristo ni kutumbukiza."

94 "A-ha," kasema, "vema." Kasema, "Sasa, wewe, ulimtumbukiza basi katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu?"

95 Nikasema, "Naam, bwana, hilo ni Yesu Kristo, hilo ndilo Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Hivyo ndivyo ni—nilivyombatiza."

96 Tena akasema, "Ulimbatiza katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu?"

97 Nikasema, "Naam, bwana. Sikuyataja hayo maneno, sasa. Nilimbatiza katika *Jina* la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, ambalo ni 'Yesu Kristo.'"

98 Akasema, "Naam, bwana, naona," naye akaliandika namna hiyo. Akasema, "Unajua, hivyo ndivyo kanisa Katoliki la mwanzoni lilivyowabatiza."

Nikasema, "Loo, je! hiyo ni kweli?"

Naye akasema, "Naam, hiyo ndiyo njia."

Nikasema, "Ni nini kilichotokea? 'Walipiga mbio vizuri.'"

99 Ndipo akasema, "Vema," akasema, "unaona," kasema—kasema, "wewe unaamini Biblia. Mungu yuko katika kanisa Lake."

100 Nikasema, "Mungu yuko katika Neno Lake, bwana, Neno Lake." Nikasema, "Je! ulisema kwamba Petro alikuwa ndiye papa wa kwanza."

Akasema, "Alikuwa."

101 "Vema," nikasema, "basi ikiwa kanisa Katoliki lazima lisome misa zake zote katika—katika Kilatini, na kadhalika, ambapo haitabadilika; basi papa wa kwanza alisema nini, katika Matendo 2:38, ambapo alisema, 'Tubuni mkabatizwe, kila mmoja wenu, katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi.'" Akasema, ikiwa utaninii. . . Nikasema, "Juu ya maungamo haya, na kadhalika," nikasema.

102 Akasema, "Vema, hivi Yesu hakuwaambia wanafunzi Wake, 'wowote mtakaowaondolea dhambi zao, wameondolewa; wowote mtakaowafungia dhambi, wamefungiwa'?"

Nikasema, "Alisema."

103 "Basi kuna shida gani na hilo? Biblia yako yenyewe inakuambia hilo."

104 Nikasema, "Basi kama mtaondoa dhambi jinsi walivyoziondoa, nitaambatana nanyi. Maana, Petro aliulizwa, yule aliyekuwa na funguo, 'Tufanye nini tuokolewe?' Yeye akasema, 'Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu.' Sasa nyinyi fanyeni namna hiyo, nami nitaambatana nanyi." Amina. Hilo ndilo

Neno. Hiyo ndiyo njia ya Mungu ya kulifanya. Walilegea katika hilo. Hiyo ni . . .

Akasema, "Vema, vema, kamwe sikuja kubishana na wewe."

105 Nikasema, "Ni nani aliyekuwa akibishana?" Mnaona? Nikasema, "Sikubishana. Sibishani. Mimi . . . wewe uliniuliza tu swali, nami nikalijibu jinsi nilivyojua kulijibu."

106 Nikasema, "Nitakuuliza moja." Nikasema, "Ulisema kwamba ninii . . . kwamba Mungu alikuwa pamoja na kanisa. Na sasa nitakupa msaada wa kukuambia, Wakristo wa mwanzoni, ukitaka kuwaita Katoliki, sawa; Petro, Yakobo, Yohana, Marko, Luka, na hao wote, wao, naam." Nikasema, "Basi katika kufuata utaratibu wa Biblia ambayo mitume hawa waliandika, sasa unamaanisha leo kwamba dayosisi yenu sasa ina mamlaka zaidi ya ilivyokuwa wakati huo, mnajua hekima zaidi? Nanyi mnajua jinsi ya kushughulikia ninii . . . ?"

"Naam, bwana. Hiyo ni kweli kabisa."

107 Nikasema, "Basi ni kwa nini ilikuwa, kwamba walipofuata amri za Yesu Kristo, walifufua wafu, walitoa pepo, wakafanya kila namna ya ishara na maajabu, nanyi hamyafanyi hayo leo? Sasa kuna shida gani?"

108 Kama kanisa lilikuwa bora zaidi wakati wa Luther, ama wakati wa Wesley, ama wakati wowote mwingine, basi ilikuwa ni huko nyuma, ni kwa nini hawakufanya kazi zao wakati huo? Mnaona? Mnaona? Hakika. Rudini kwenye Neno!

109 Samsoni alisimama pale, amevuliwa nguvu zake. Bali, mnajua, kulikuwa na kitu fulani (Ninataka kuharakisha) Wafilisti hawakutambua, wakati Samsoni alipokuwa amesimama pale akiwazia haya yote.

110 Laiti ningaliweza kuuchukua ulimwengu wa Kipentekoste na kuwaweka pembeni mahali fulani, niwaache wawazie hivyo kwa kitambo, kuwazia tu mambo haya mazuri. Tuko wapi sasa na lundo hili kubwa la madhehebu? Kila moja likipinga lile lingine. Wa Umoja wanapinga wa Uwili, wa Uwili wanapinga wa Utatu, na kadhalika, wote, hivyo tu ndivyo ilivyo. Hiyo haipaswi kuwa hivyo. Haipaswi kuwa hivyo. Tunapaswa kurudi nyuma, na tuungane pamoja na kulitatua juu ya msingi wa BWANA ASEMA HIVI.

111 Kuna shida gani na manabii kanisani? Neno la Bwana linapaswa kuwajia manabii. Na kama nabii anayedai kuwa nabii, naye atakana Kweli hii katika Biblia, kulingana na Neno, yeye si nabii. Sasa, tunapaswa kuwa na karama hizi kutuweka katika utaratibu, kutuweka katika utaratibu. Lakini hapo, kwa njia moja au nyingine, tuliziondokea zote. Nao wanasimama, wamefungiwa kwenye kona.

112 Hapa alisimama Samsoni, amesimama kwenye kona, akiwazia yote yaliyokuwapo. Nao hawa Wafilisti wakisimama

huko juu, wamewakumbatia hawa wanawake, wakiangalia chini, wakiteuka na wamelewa, na kusherehekea ushindi dhidi ya mtumishi wa Yehova. Loo, jamani, hilo si linatuma kitu kupitia ndani yako, kuwazia hilo, ushindi dhidi ya mpango wa Yehova! Naam, wakisimama pale na mungu samaki. Dagon alikuwa ndiye mungu samaki. Nao walikuwa wakiteketeza kafara. Uhai wa wanadamu ulitwaliwa, ilibidi mtoto mdogo afe kwa ajili ya sadaka, wanamchoma upanga, kupitia moyo wake, kwa ajili ya sadaka. Nao walikuwa pale, wakifanya sherehe hii kubwa juu ya ushindi juu ya Yehova.

113 Nalo kanisa usiku wa leo, kama kundi la Wafilisti, wanalicheka kwa bezo wazo la kwamba Baraza la Makanisa, baada ya kitambo kidogo, litafunga kila kanisa ambalo si mshiriki wake. Samsoni, kamwe usikate nywele zako! Dumu sawa na Neno hilo. Sijali kile kinachotendeka, wewe dumu papo hapo pamoja na Neno hilo. Usichangamane katika hilo.

114 Samsoni akaanza kuwazia, "Sijui kama kuna uwezekano?" Sasa alisema, "Ninajua nywele zangu zimekua, bali mimi ni kipofu. Huenda kukawa na uwezekano wa uamsho mwingine. Kuna uwezekano."

115 Akamwambia huyo mvulana mdogo, "Weka mikono yangu kwenye mwimo. Je! hii ndiyo miimo inayoshikilia jengo lote?"

"Naam."

"Na unasema wafalme na watu wote mashuhuri wako juu?"

"Naam."

116 "Nimechoka. Imekubidi kufanya hivyo, kunifanya kufanya vitimbi vingi na kadhalika! Hivi utaweka tu mikono yangu juu ya mwimo?"

117 Ndipo akaweka mikono yake juu ya mwimo, na kusimama katikati yake, labda namna *hii*. Ndipo akasimama hapo na mikono yake kwenye miimo. Wafilisti, wakisherehekea na kuwa na wakati mzuri sana, walisahau kumwangalia. Loo, jamani!

118 Lakini yeye akaanza kuwaza, "Mungu angali ni Mungu. Ninajua Yeye angali hivyo. Nimemjaribu. Nimemtia katika majaribu. Ninajua angali ni Mungu. Ni mimi nimekosea. Mimi ndimi nimetenda dhambi." Hawakuona machozi yakitiririka kutoka kwenye hayo mashimo ya macho yaliyopofuka, yakidondoka chini kutoka kwenye shavu lake. Hawakuona midomo yake ikicheza. "Bwana, nimefanya kosa. Jalia nife na hawa Wafilisti."

119 Alitaka Neno la Mungu lidhihirishwe mbele ya huyo Yezebeli, zaidi ya alivyotaka uhai wake mwenyewe. Loo, laiti shauku hiyo ingekuja kwa kanisa tena! Naam. Hakuwa anaombea utaratibu mpya, dhehebu jipya, ila kwamba Neno la Mungu liweze kujulikana tena; ahadi aliyokuwa nayo wakati mmoja, iweze kumrudia tena. Alikuwa anajua kile ambacho

kingetukia ikiwa maombi yake yangejibiwa, bali alikuwa tayari na bidii thabiti. Loo, laiti kanisa lingaliweza tu kuwa namna hiyo! Ndipo akalia kwa sauti kuu!

120 Pole pole alikuwa anaomba, "Inawezekana, Bwana. Inawezekana. Ninasimama hapa, mwili wangu wote mkubwa ungali pamoja. Nipo hapa, nywele zangu zimekua. Bali nisingeweza kuona namna ya kuwapiga tena, maana macho yangu yamepofuka. Nisingeweza kuona mahali nilipokuwa ninaenda. Bali inawezekana kwamba—kwamba Wewe ungejalia litendeke tena, Bwana, kuonyesha nguvu Zako."

Alilia kwa sauti kuu, "Mara moja zaidi, Bwana, mara moja tu zaidi!"

121 Loo, laiti kanisa lingeweza tu kulia hilo, "Mara moja zaidi, Bwana, jalia tuone nguvu Zako!"

122 "Mara moja zaidi!" Ndipo wakati alipolia na kumwomba Mungu, ninaweza kuona misuli hiyo ikianza kutanuka. Kila mshipa mwilini mwake ukaanza kugeuka. Roho Mtakatifu alikuwa anakuja juu yake wakati huo. Akanyosha mikono yake tena, huku nguvu za Roho Mtakatifu zikiwa juu yake, jengo likaporomoka. Biblia ilisema, "Aliwaua wengi siku hiyo kuliko wale alioua katika siku zake zote." Alitimiza agizo ambalo alipewa na Mungu, wakati huo. "Mara moja zaidi!"

123 Daima imekuwa hivyo wakati nguvu za Mungu zikija, miundo mikubwa ya itikadi huanguka. Ushindi mkubwa zaidi Samsoni aliopata dhidi ya adui wake ulikuwa kwenye wakati wake wa mwisho.

124 Sasa hebu niseme hili, katika kufunga tu. Pentekoste, je! tunaweza kusimama mahali pa madhehebu haya makubwa, je! tunaweza kusimama mahali pa Hollywood na mambo haya mengine yote yanayotutenganisha na upendo wa Mungu ulio ndani ya Kristo, na je! tunaweza kusimama hapo na kutubu, na kulia kwa sauti kuu tena, "Bwana, mara moja tena tufanye pentekoste! Mara moja tena, Bwana, mara moja tena tufanye pentekoste! Mara moja tena onyesha nguvu Zako ndani yetu, Bwana! Mara moja tu zaidi"?

125 Sikilizeni, mwangamize adui wako kabla adui wako hajakuangamiza. Atakuangamiza. Rudisha mikutano ya mtindo wa kale na kitu hicho. Na, loo, achana na Delila, achana na ulimwengu, kitu kile ambacho hukuvuta kando kuingia katika mambo madogo usiyopaswa kuingia. Na mambo madogo, shida zinainuka kanisani, nawe hutavumilia marekebisho kwa sababu haikubidi kufanya hivyo; unaweza kuondoka uende kanisa jingine, na mambo kama hayo. Katika siku za mwanzoni, mtu alipokosa kuambatana na Neno la Mungu, walimbeba kumtoa nje, amekufa.

126 "Turejeshe pentekoste!" Sio maonyesho ya Hollywood, bali kumgeukia Mungu kwa moyo wote ndicho tunachohitaji. "Mara moja zaidi, Ee Bwana, mara moja zaidi!"

127 Laiti ningaliweza kuona hilo likitendeka, laiti maskini macho yangu yanayofifia yangeweza kuangalia tena na kuliona kanisa hilo likisahau tofauti zake! Laiti ningaliweza kuona mfumo huo wa kidhehebu ukiporomoka, na kuutupa moja kwa moja pajani mwa hilo Baraza, na kusema, "Hatutaki uhusiano wowote nao! Hatutapoteza haki zetu za mzaliwa wa kwanza!" Laiti ningaliweza kuona wa Utatu na wa Umoja, na wote, wakiungana na kusema, "Ndugu, hebu turudi mahali tulipomwacha. Hebu turudi mahali tulipoanza kulalamikiana mmoja kwa mwenzake, moja kwa moja kurudi juu ya somo la ubatizo wa maji, na kurudi moja kwa moja na kuchukua njia ya Biblia kwa ajili yake," ndipo tupige makelele, "Mara moja zaidi, Bwana, mara moja zaidi!" Na kuondoa maonyesho haya yote. . .na wengi wa jamaa hawa jukwaani nao hawajui kuhusu Mungu zaidi ya vile sungura anavyojua kuhusu viatu vya theluji, na hawa wanawake wakiwa na nguo zinazobana sana hata ngozi yao iko nje, wakitembea huku na huku jukwaani, wakipiga makofi na kuruka namna hiyo, kama kundi la maonyesho ama kitu kingine.

128 "Mungu, turejeshe kwenye Roho Mtakatifu na nguvu, na madhihirisho ya Neno! Mara moja zaidi, Bwana, mara moja zaidi!" Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] "Bwana Mungu, mara moja zaidi, mara moja zaidi jalia nione Uwepo wa Yesu Kristo akitembea kupitia kwenye kanisa, jalia nione nguvu Zake na ahadi Yake ikidhihirishwa mbele yetu. Mara moja zaidi, Bwana, mara moja zaidi! Mungu, turehemu, tusaidie!"

129 Mnaona kile vitu hivi vingine hutuletea? Huua ninii yenyewe. . .huondolea mbali asili ya Kristo, kutoka kwenye kusanyiko, kutoka kwenye—kutoka kwenye kanisa, kwenda mbali na watu. Tunapaswa kushikamana pamoja sana hata hakungekuwa na chochote kitakachotutenganisha kutoka kwenye Neno hili na upendo wetu mmoja kwa mwenzake.

130 Yesu Kristo yupo hapa. Yeye ni Baba yetu. Yeye ni Mama yetu. Yeye ni Mponya wangu. Yeye ni Mfalme wangu. Yeye ni Mungu wangu. Yeye ni Uzima wangu. Yeye ni furaha yangu. Yeye ni amani yangu. Yote yaliyoko, Yeye ndiye, kwangu mimi. Yeye ni yote kwa yote kwangu mimi. Yeye yupo hapa sasa.

131 Anataka kulirejesha kanisa mahali pale. Sijui kama tungeweza kulia, "Mara moja zaidi, Bwana," na kuyaacha ma—machozi ya toba kudondoka kutoka kwenye mashimo ya macho yetu yaliyopofuka? Mimi sizungumzii kanisa hili hasa. Huu unanaswa kwenye kanda, mnaona, hapa, huu utaenda kote ulimwenguni. Hebu nanii wetu—hebu watu wetu warudi kwenye

hilo tena, hebu irudi kwenye mahali ambapo tungeweza kuitisha tena m—mkutano kama tulizoea kuwa nao.

132 Chukua tu hata miaka kumi ama kumi na tano, nyuma, angalia jinsi imedidimia tangu wakati huo, angalia jinsi imeenda chini, chini, chini. Imefikia hata karibu ni aibu, mtu unajisikia kuaibika, karibu, kuzungumza kuhusu uponyaji wa Kiungu, kumekuwa na aibu nyingi sana zimeletwa juu yake; nena kuhusu Roho Mtakatifu, wakati aibu nyingi sana zimeletwa juu Yake. Hiyo ni kweli. Si kosa la Mungu. Ni Samsoni ambaye ameziacha kanuni za Neno la Mungu, na ameweka kitu kingine cha badala, na kuliacha dhehebu limnyoe, na kumshawishi kuingia ndani ya hilo.

133 Ninawaambieni, ndugu yangu, dada, nisipowaona tena upande huu wa—wa Hukumu kuu ya Mungu, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Neno Lake, kwangu mimi, ni Uzima. Yeye yupo hapa sasa. Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ninajua Yeye yupo hapa.

134 Basi jambo la pekee unalopaswa kufanya, kujua kwamba Yeye yupo hapa, ni kujiondosha njiani. Mnaona? Mradi ungali kwenye njia, basi Mungu hawezi kukufanyia lolote. Unapowaza mawazo yako, basi mawazo ya Mungu hayana nafasi. Bali ikiwa utaacha kuwaza mawazo yako, na kuwaza mawazo Yake! "Mawazo Yangu si mawazo yako," Yeye alisema. "Ikiwepo sifa yoyote, ukiwapo na wema wowote, yatafakarini hayo." Si yale kanisa fulani litakayosema kulihusu, bali yale Mungu aliyosema kulihusu!

135 Kama maskini mama huyu aliyelala hapa, akitetemeka katika kitanda hiki cha wagonjwa. Mwanamke huyo atalala hivyo maisha yake yote, isipokuwa aweze kuelekeza ninii yake—imani yake moja kwa moja kwa Yesu Kristo. Na haijalishi ni nini kinachotokea, ikifunuliwa kwake, basi hakuna kitu kitakachozuia uponyaji. Hiyo ni kweli. Bali ukielekeza ninii yako . . . Inategemea yale unayowazia.

136 Iwapo utaamini tu na kuwa na imani, Mungu anaweza kukufanyia chochote. Na jambo kuu zaidi ambalo Yeye anaweza kukufanyia, usiku wa leo, ni kuirudisha nafsi yako moja kwa moja katika Uwepo wa Utu Wake. Moja kwa moja mpaka pale ambapo kila mtu humu ndani . . .

137 Wazia tu, vipi kama Roho Mtakatifu angekuwa na kila mtu humu ndani chini ya mamlaka Yake? Wazia kile ambacho kingetukia usiku wa leo, wazia kile ambacho kingetukia Shreveport kufikia wakati huu kesho usiku! Wangekuwa na vichwa vya habari kila mahali, "Kundi la watu liliingia kichaa. Walikuwa wakiwaponya wagonjwa na kufufua wafu. Wanafanya kila namna ya mambo huko chini Shreveport, Louisiana, Marekani, Amerika." Wangekuwa nayo kwenye televisheni, juu

ya kile walichokuwa wakifanya, kama Roho Mtakatifu angeweza kuchukua utawala mkamilifu.

138 Mbona asichukue mamlaka? Yeye anataka kufanya hivyo. Yuko tayari kuchukua mamlaka. Anangojea. "Vema," unasema, "Nimemwomba mambo mengi sana, ninachukia tu kumwomba kupita kiasi." Ombeni kwa wingi, furaha yenu iwe timilifu!

139 Ungeweza kuwazia samaki mdogo, mwenye urefu wa nusu inchi, huko katikati ya Pacific, akisema, "Heri ninywe maji haya kwa unyimifu, huenda nikayamaliza, siku moja"? Hivi ungeweza kuwazia panya mdogo yapata ukubwa *huo*, katika maghala makubwa ya Misri, awazie, "Nitajiruhusu kula punje moja kwa siku, maana huenda nikamaliza kabla ya mavuno yafuatayo kufika"? Loo, jamani! Sasa gawa hilo mara bilioni mia moja, na hivyo ndivyo ilivyo rahisi kwako kumaliza rehema za Mungu na neema na nguvu kwako, ikiwa tu utaamini, unaweza tu kujiacha mwenyewe. . . Vema, samahani mimi . . . hiyo ni kusema, huwezi kummaliza Yeye.

140 Yeye ndiye chemichemi isiyomalizika ya Uzima wa Milele, hapa usiku wa leo kudhihirisha ahadi yoyote ya Kiungu ya Biblia Yake, kwa mtu yeyote atakayeamini Hiyo. Amina. Naam, bwana. Kitu cha pekee unachofanya ni kunywa. Njoo kwenye chemichemi na unywe. Kunywa mpaka utosheke. Huwezi kummaliza Yeye. La, bwana. Yeye kwa hakika ni asiyemalizika, nawe unaweza ukanywa tu na kunywa na kunywa. Unaweza kunywa ukaingiza uponyaji wako. Unaweza kunywa ukaingiza wokovu wako. Njoo tu unywe. "Aliye na kiu na aje anywe." Amina. Na—na—na—najua Yeye yupo hapa, nami ninajua Yeye atafanya makuu, kwa wingi ikiwa tu tutamwacha Yeye afanye hayo.

141 Ndio kwanza nione jambo fulani likitendeka. Na si—sitaki kuanzisha moja ya ibada za namna hiyo, mnaona, ya maono, kwa sababu ni—ninazungumza kuhusu kitu kingine. Mnaona, ninazungumza kuhusu wewe kuja, si kwa uponyaji wa kimwili, bali kuja kwenye—kwenye . . . Punde tu wanapoanza kufanya hilo, sasa hiyo ni ninii tu . . . Mnaona, punde tu nilipoanza kujituliza basi, ili kuondoka, muda si muda wajua, watu wakashika, mwajua, unahisi hiyo ikiingia.

142 Hapa, ninaweza kuwaambieni. Mtu yule anayeketi pale nyuma, akiwa na mvulana wa mpwa wake mwenye shida hiyo ya nyonga. Kama ataamini, Mungu atamponya na kumpa afya. Je! unaamini kwamba Yeye angeweza kumponya na kumpa afya? [Ndugu huyo anasema, "Amina."—Mh.] Kama unaamini, vema basi Mungu atamponya. Unaona? Kweli kabisa. Amina.

143 Huyu hapa mwanaume ameketi papa hapa, akiniangalia moja kwa moja. Anaiombea familia yake. Yeye kwa kweli hatoki hapa. Anatoka Carolina ya Kusini. Bw. Dixson. Lakini ikiwa ataamini tu kwa moyo wake wote, Mungu atamjalia

baraka hiyo. Je! unaamini hilo, bwana? Mimi ni mgeni kabisa kwake. Sijawahi kumwona, maishani mwangu. Amina. Sijawahi kumwona, maishani mwangu.

144 Lakini je, mnaona ninalomaanisha? Ni kitu gani? "Hiyo inafanya kazi namna gani, Ndugu Branham?" Wakati Ndugu Branham anapoweza kuondoka njiani! Naam, bwana. Ninapoweza kuondoka njiani, ndipo Yesu Kristo anapoingia.

145 Jambo jingine, moja kwa moja kutoka kwake, yupo mwanaume mwingine aliyeshika Moto, naye anatoka Carolina ya Kusini, pia. Hiyo ni kweli. Ninaiona Hiyo ikining'inia moja kwa moja juu yake. Hiyo ni kweli kabisa. Anamwombea ndugu aliye mlevi wa pombe. Hiyo ni kweli kabisa. Sikilizeni. Wewe ni Ndugu Holmes. Je! unaamini kwamba Mungu . . . Je! hilo ni jina lako? Mungu hufanya . . . Mungu atakujalia.

Mnaona ninalomaanisha? "Mara moja zaidi, Bwana, mara moja zaidi!"

146 Hebu tusimame kwa miguu yetu, kila mtu. Lieni, Wapentekoste, inueni mikono yenu, "Mara moja zaidi, Bwana! Mara moja zaidi, Bwana, mara moja zaidi!" Haleluya! Sijui la kufanya, lakini ipo hapa. Hebu tulie, kwa nia moja, "Mara moja zaidi, Bwana!" Lieni kwa sauti, "Mara moja zaidi, Bwana! Mara moja zaidi, Bwana! Mara moja zaidi, Bwana, tuma Nguvu Zako, tuma baraka Zako. Mtume Roho Mtakatifu juu yetu, kama upepo mkuu unaovuma, na ujaze kila nafsi iliyoko hapa ndani, upya." Utukufu kwa Mungu! Aminini hilo kwa moyo wenu wote. "Mara moja zaidi, Bwana, mara moja zaidi!" Haleluya!

147 Kulewa kwa Roho! Ikiwa Roho Mtakatifu anaweza tu kujimimina ndani yako mpaka uwe umelewa sana unasahau jina lako ni nani, mpaka usahau mashaka yako yote; kukulewesha sana na Roho mpaka usahau mashaka yako, amina, ndipo unaweza kufika mahali na Mungu. Ndipo kilio, "mara moja zaidi," kinapaa juu kutoka kwa uaminifu, na halafu mwingine. Haleluya! Umejazwa na Roho Mtakatifu, hawa wamelewa kwa Roho; haki ya Mungu na utakatifu, na nguvu, hukulewesha sana mpaka unajisahau. Wewe si kitu, kuanzia. Kumbuka, Mungu anataka aje ndani yako. "Mara moja zaidi, Bwana, mara moja zaidi! Mara moja zaidi, Bwana, mara moja zaidi!"

148 Loo, Wapentekoste, Wapentekoste, kimbilieni maisha yenu! Kuna muda mfupi tu uliosalia. Wakati umeenda kuliko mnavyodhania. Nisiposema neno lingine kutoka kwenye mimbara hii, kumbukeni, kimbilieni maisha yenu! Wakati umeenda kuliko mnavyodhania. Ninamhisi Roho Mtakatifu juu yangu, akisema, "Sema hilo tena." Kimbilieni maisha yenu! Kumechelewa kuliko mnavyodhania.

149 Mara moja zaidi, Bwana, mara moja zaidi ijaze Maskani hii ya Uzima na Uzima wa Milele, kila mshiriki hapa ndani. Pia jalia Utukufu wa Bwana ushuke juu ya kusanyiko hili, Bwana Yesu.

Haleluya! Haleluya! Ninamwamini Mungu. Mara moja zaidi, Bwana, mara moja tena jalia watu wajisahau kuwa ni akina nani. Jalia mtu asahau kutokuamini kwake, hata tuweze kulia, "Mara moja zaidi, Bwana, mara moja zaidi!"

Je! mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

150 Ee Mungu, Baba wa Mbinguni, tupe uamsho ndani ya nafsi zetu, Bwana. Tunaona ta—ta—taa zinajaa moshi, Moto kwenye madhabahu unazimika. Ee Bwana Mungu, angalia chini kwenye taifa hili lililolaaniwa na dhambi, lakini, Bwana, usiwasahau watu Wako. Watu hapa wamejitahidi kwa miaka, Bwana, kukujengea Wewe milki hii ndogo. Maskani ya Uzima ilijengwa, Bwana, kwa ajili ya—ya kituo cha kuokolea nafsi, kwa ajili ya uamsho. Ee Mungu, mara moja tena mimina Nguvu Zako Takatifu ndani yake. Mjaze kila mshiriki, ondolea mbali kila tofauti. Itume mvua ya Moto Mtakatifu wa Mungu na uzitie nuru nafsi zetu, Bwana, kwa Uwepo wa Yesu Kristo. Jalia watu wasizame sana katika kutokuamini, hata waweze kuona kwamba Wewe upo hapa pamoja nasi; na Wewe ni Neno, na Mtambuzi wa mawazo ya moyoni, kama vile Biblia imethibitishwa sana kwetu, mara na mara tena. Bwana Mungu, jalia tuamke katika hisia zetu, kujua kwamba Roho wa Mungu yuko miongoni mwetu. Tujalie, Baba. Ninaikabidhi Kwako, pamoja na mimi mwenyewe. Amina.

151 Ndugu, dada, sijui, katika Biblia yangu, kitu chochote kingine Mungu alichoahidi kufanya kabla ya Unyakuo wa Kanisa. Sijui. Mnawaza kuhusu alama ya mnyama, kuja; nimewaambia, ni, tayari wameipokea. Mnaona? Kitu kingine kilichosalia ni kwa ajili ya Unyakuo wa Kanisa. Unaweza kuja wakati wowote, na usivunje Maandiko yoyote kwenye Biblia, kadiri nijuavyo mimi. Mungu anajua hiyo ni kweli. Naam, bwana. Wakati umekaribia. Wakati umeenda kuliko tunavyodhania.

152 Hebu tufunge tu macho yetu, na tuimbe, *Nampenda*. Labda, kama tutamwabudu na kumsifu, labda Yeye atatenda jambo. Nimeomba juma hili lote, kuona ushindi mkuu katika maskani hii. Niliomba kabla ya kuja hapa. Ninao watu wanaoombea jambo hili. Loo, kuna—kuna maombi yanayoendelea kwa ajili ya jambo hili. Ninajaribu kuamini kwa moyo wangu wote. Hebu tuamke, upesi sana. Hebu tumwabudu tu na kumsifu, huku tukiimba huo sasa macho yetu yakiwa yamefumbwa na mikono yetu kwa Mungu.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

153 Sasa wakati tukiimba aya inayofuata, peana mikono na mtu fulani karibu nawe, ndugu yako Mkristo, useme, "Mungu akubariki," sasa wakati tukiuimba.

> Nampenda, na. . .(Kama mnapendana ninyi kwa ninyi, hamwezi kujizuia kumpenda Mungu.)
> Kwani kwanza. . .
> . . .wokovu
> Mtini kal-. . .

154 Sasa hebu tuseme, "Haleluya!" "Haleluya!" Sema hilo tena, "Haleluya!" Tena, "Haleluya!" Msifuni Mungu wetu!

> Nampenda, nampenda kwani. . .

Ndugu Don, uko tayari?

*Mara Moja Tu Zaidi, Bwana* SWA63-1201E
(Just Once More, Lord)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, tarehe 1 Desemba, 1963, katika Maskani ya Life kule Shreveport, Louisiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org